

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21), MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22-2025/26) PAMOJA NA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.

Ofisi ya Bunge.

S.L.P 941

DODOMA

Februari, 2021

1.0.	UTANGULIZI.....	1
2.0.	TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21).....	2
2.1.1.	Ukuaji wa Pato la Taifa.	3
	Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha Miaka 4.....	3
2.1.2.	Wastani wa Pato la Kila Mtu	4
2.1.3.	Mfumuko wa bei	5
2.1.4.	Mwenendo wa viwango vya ubadilishaji wa fedha	6
2.1.5.	Deni la Serikali	7
2.1.6.	Mwenendo wa Huduma za kibenki na viwango vya riba	8
2.2.	Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/17 – 2020/21.	9
2.3.	Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21)	10
2.3.1.	Sekta ya Miundombinu	10
2.3.1.1.	Barabara	10
2.3.1.2.	Reli.....	12
2.3.1.3.	Usafiri wa Anga.....	13
2.3.2.	Sekta ya Nishati	13
2.3.3.	Sekta ya Kilimo	14
2.3.4.	Sekta ya Viwanda na Biashara	16
2.3.5.	Sekta ya Ardhi na Mazingira	18
2.3.6.	Sekta Utalii	19
2.3.7.	Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi	19
2.3.8.	Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu	21
2.3.8.1.	Afya.....	21
2.3.8.2.	Elimu.....	23
2.3.8.3.	Maji	24
2.3.8.4.	Mapitio ya Sera ya Kuondoa Umaskini.....	24

3.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22- 2025/26).....	25
3.1. Malengo na Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.....	26
3.2. Uchambuzi na Vyanzo vya Mapato vya ugharamiaji wa Mpango.....	26
3.3. Upatikanaji wa Mapato na Mwenendo wake	28
3.4. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati (Flagship Project).....	29
3.5. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili miradi ya maendeleo.....	29
3.6. Sekta za Huduma ya Elimu na Afya	30
3.6.1. Sekta ya Elimu.....	30
3.6.2. Sekta ya Afya.....	32
3.7. Tathmini, Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango	32
4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA (2021/22-2025/26).....	33
4.1. Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ..	33
4.2. Sekta ya Ujenzi	34
4.3. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu	34
4.4. Ukarabati na ujenzi wa Viwanja vya Ndege.....	35
4.5. Mzingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji.....	35
4.6. Ushirikishwaji wa Watanzania katika Miradi ya Maendeleo na Uwekezaji nchini (Local Content)	36
4.7. Uzingatiaji wa Mapinduzi ya Kidijiti (Digital revolution) katika Mipango ya Maendeleo.....	36
4.8. Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Bahari Kuu	37
4.9. Maboresho katika kituo cha uwekezaji	37
5.0. MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.	38
5.1. Utangulizi	38
5.2. Utekelezaji wa Bajeti katika Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21.....	39
5.3. Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22	40
6.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22.....	42
7.0. MAONI YA JUMLA.....	45
8.0. HITIMISHO.....	47

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TATHMINI YA
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO (2016/17-
2020/21), MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA
MIAKA MITANO (2021/22-2025/26) PAMOJA NA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA
MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/17-2020/21), Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26) pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inawasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kujadiliana kwa kina na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”** pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025 ulipangwa kwa kufuata mfumo wa kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano Mitano, hivyo tulianza kwa kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/2012 -2015/2016) uliokuwa na dhima ya **“Kufungulia**

fursa ya Ukuaji wa Uchumi” (Unleashing Tanzania’s Latent Growth Potential); ukafuata Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/2017 – 2020/21) wenye dhima **“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”(Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development)** na sasa tunajielekeza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022- 2025/2026) wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda Kwa Maendeleo ya Watu” (Realising Competitiveness and Industrialisation for Human Development).**

Mheshimiwa Spika, tathmini zinaonyesha kuwa utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na huu wa Pili tunaomaliza kutekeleza sasa umesaidia katika kujenga msingi wa Uchumi imara na hivyo kupelekea kufanikiwa kutimiza azma ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ya kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati (***Lower - Middle Income Country***) mwaka 2020.

2.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21)


2.1. Viashiria vya Uchumi Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ndio mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2016/17-2020/21), Kamati iliona ni vema kufanya tathmini na mapitio wa hali ya ukuaji wa Uchumi wa Taifa katika vipindi vya utekelezaji wa Mpango wa Pili (Miaka 4) kwa kuangalia mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi pamoja na utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Pili na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Lengo ni kuona kwa kiasi gani tumeweza kufikia malengo tuliojiwekea pamoja na kuona changamoto zilizojitokeza na hivyo kuwa na nafasi ya kubainisha nini kifanyike kwenye Mpango wa Tatu tunaotegemea kuanza kuutekeleza.

2.1.1. Ukuaji wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 4 (2016-2019) ukuaji wa Pato la Taifa umeendelea kuwa imara, ambapo Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa **asilimia 6.9**. Ukuaji huu umekuwa ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji hasa katika miundombinu ya usafirishaji na nishati; uchimbaji madini; uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato na kubana matumizi yasiyo ya lazima pamoja na hali nzuri ya hewa ambayo imepelekea kuongezeka kwa mazao katika sekta ya kilimo. Hata hivyo, pamoja na ukuaji huu unaoridhisha bado nchi haijaweza kufikia malengo yake ya ukuaji wa uchumi wa zaidi ya **asilimia 8** kama ilivyoainishwa katika malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiwango ambacho kingesaidia kupunguza umaskini nchini kwa kasi zaidi.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha Miaka 4



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kati ya kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 takwimu zinaonesha kuwa sekta zilizokuwa na ukuaji wa juu ni ujenzi (**asilimia 14.4**); uzalishaji (**asilimia 8.3**), usafirishaji na uhifadhi wa

mizigo (**asilimia 8.2**); uchimbaji wa madini na mawe (**asilimia 8**); habari na mawasiliano (**asilimia 6.2**). Hii ina maana kwamba ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa unachochea na shughuli za ujenzi, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma. Kwa upande wa wa sekta ya kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) ukuaji wake umekuwa sio wa kuridhisha licha ya kuwa inaajiri watanzania wengi (**asilimia 66**). Takwimu inaonyesha kuwa sekta hii imekuwa kwa wastani wa chini ya **asilimia 5**, ukuaji ambao ni chini ya malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa kukua kwa **asilimia 7.6**. Vilevile uchangiaji wa sekta hii katika Pato la Taifa umeshuka kutoka **asilimia 29.0** mwaka 2016 hadi **asilimia 26.6** mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020 Pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa **asilimia 4.7** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 6.9** mwaka 2019. Kushuka kwa ukuaji huku kumechangiwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu uliochangiwa na mafuriko yaliyotokea katika maeneo mengi nchini pamoja mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao umeathiri ukuaji wa uchumi wa nchi nyingi duniani ikizingatiwa kuwa uchumi wetu pia unategemea ukuaji wa uchumi wa dunia. Hivyo, kutokana na mwenendo huu tategemea ukuaji wetu wa Pato la Taifa kuwa chini wa wastani wa **asilimia 6.9** kwa mwaka 2020/21.

2.1.2. Wastani wa Pato la Kila Mtu

Mheshimiwa Spika, Kutokana na ukuaji imara wa uchumi kwa wastani wa zaidi ya **asilimia 6** katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, mwezi Julai 2020 Benki ya Dunia iliitangaza Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipato cha kati cha chini. Hatua hii ilitokana na kuongezeka kwa pato la mtu (GNI) kutoka **shilingi 2,452,406 (sawa na dola za Marekani 1,020)** mwaka 2018 hadi **shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,080)** mwaka 2019, kiasi hicho ni juu ya kiasi kilichowekwa na Benki ya Dunia cha **dola za Marekani 1,036** ili nchi iweze kufikia hadhi ya kipato cha kati cha

chini (Lower-middle income status). Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha Nchi imefikia lengo la kuwa nchi ya kipato cha kati miaka mitano kabla wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.


Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamechangiwa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa wastani wa **asilimia 6.9** kwa kipindi cha miaka minne (2016-2019); utegemezi wa kibajeti kutoka **asilimia 14.0** ya bajeti halisi mwaka 2014/15 hadi **asilimia 9.3** mwaka 2019/20; ujenzi wa miundombinu muhimu ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi (miundombinu, umeme, elimu, afya na maji) pamoja na utawala bora. Aidha, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 23 za Afrika zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini.

2.1.3. Mfumuko wa bei

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja **asilimia 4.4** katika kipindi cha miaka minne 4 (2016-2019) na hivyo kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa kiwango cha kutokuzidi **asilimia 5** ya Mfumuko wa Bei. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kudhibiti mwenendo wa ukuaji wa mfumuko wa bei kwa utekelezaji thabiti wa sera za fedha na kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Kwa kiasi kikubwa Mfumuko wa bei nchini huchangiwa kwa kiwango kikubwa na upatikanaji wa chakula nchini na nchi jirani pamoja na bei ya mafuta katika soko la dunia. Kwa kuwa Nchi yetu haina uwezo wa kuamua bei ya mafuta katika soko la duniani ni vema tukajikita katika kuhakikisha Taifa linakuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya watu wake na kuweza kuuza kwa majirani zetu.

Kielelezo Na.2: Mfumuko wa Bei




Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.

2.1.4. Mwenendo wa viwango vya ubadilishaji wa fedha

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka 4 iliyopita thamani ya Shilingi imeendelea kuwa imara dhidi ya Sarafu kubwa. Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2019/20 inaonyesha kwamba hadi mwishoni mwa mwaka 2016/17 kiwango cha kubadilisha dola moja ya Kimarekani ilikuwa ni **Shilingi 2,230.1** na mwishoni mwa mwaka 2019/20 dola moja ya marekani ilibadirishwa kwa **Shilingi 2,295.5**. Utulivu wa thamani ya fedha yetu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa urari wa biashara kati yetu na washirika wetu wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Utulivu huu umepelekea uwepo wa fedha za kigeni za kutosha na hivyo kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 5.6** (Desemba, 2020) na hivyo kumeiwezesha nchi yetu kuendana na vigezo vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) vya miezi 4.5. Mafanikio haya yanastahili pongezi.

Kielelezo Na.3. Mwenendo wa Viwango vya Riba



Chanzo: Wizara ya Fedhana Mipango.


2.1.5. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia **shilingi trilioni 59** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 54.8** kipindi kama hicho mwaka 2019 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 7.6**. Kati ya kiasi hicho deni la ndani lilifikia **shilingi trilioni 16.2** na deni la nje **shilingi trilioni 42.8**. Ongezeko la deni limetokana na Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2020, deni letu ni himilivu kwa vigezo vyote vya Kimataifa na hivyo, Nchi yetu ina uwezo wa kukopa ndani na nje, na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi. Pamoja na kwamba deni hilo ni himilivu kwa viashiria vyote muhimu, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali ione haja ya kujipima uhimilivu wake kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa Pato la Taifa ambacho kwenye mpango hakijaripotwa. Hii ni kwa sababu deni la Taifa huhudumiwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima (*first charge*) katika

matumizi ya Serikali. Vile vile Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa *credit rating* ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi.

Kielelezo Na.4. Mwenendo wa Deni la Serikali.



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango.

2.1.6. Mwenendo wa Huduma za kibenki na viwango vya riba

Mheshimiwa Spika; Katika kipindi cha miaka minne (2016 - 2019), viwango vya riba katika masoko ya fedha vimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti. Viwango vya riba za dhamana za Serikali umepungua kutoka **asilimia 16.7** mwaka 2016 hadi **asilimia 7.71** mwaka wa fedha 2019. Aidha, Riba za mikopo kwenye mabanki ya biashara katika kipindi hicho ziliongezeka kutoka **asilimia 15.96** mwaka wa fedha 2016 na kufikia **asilimia 16.97** mwaka 2019. Riba za amana za akiba zilipungua kutoka **asilimia 3.35** katika mwaka 2016 na kufikia **asilimia 2.44** mwaka 2019. Hatua hii ilifikwa baada ya Benki Kuu kutekeleza sera ya fedha kwa kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kilichotakiwa kuwekwa Benki Kuu na Mabanki (Statutory Minimum Reserve) kutoka **asilimia 7** kwenda **asilimia 6** ya amana zote za kila Benki. Vilevile Benki kuu ilipunguza

kiwango cha riba kwa Mabenki yanapokopa Benki Kuu (Discount Rate) kutoka **asilimia 12** kwenda **asilimia 9** na mwaka 2020 ilipunguzwa na kufikia **asilimia 5**, lengo lilikuwa kuongeza ukwasi ili kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi na hatimaye ukuaji wa uchumi. Hata hivyo pamoja na hatua hizi zilizofanywa na Serikali kupitia Benki Kuu, bado mabenki ya biashara yamekuwa yakitoa mikopo kwa sekta binafsi katika kiwango cha riba kisichovutia mkopaji. Aidha, bado tofauti kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja imekuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama za fedha kwa wawekezaji katika sekta binafsi.

2.2. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/17 – 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ulikadiriwa kugharimu **Shilingi trilioni 107**, sawa na wastani wa **Shilingi trilioni 21.4** kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano. Sekta ya umma ilitarajiwa kuchangia kiasi cha **Shilingi trilioni 59**, huku sekta binafsi ikitarajiwa kuwekeza **Shilingi trilioni 48**.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa miaka minne ya kwanza umebaini kuwa sekta ya umma ilichangia Shilingi **trilioni 34.9**, sawa na **asilimia 76.5** ya lengo la miaka minne ya **Shilingi trilioni 45.6**. Aidha, katika kipindi hicho, Sekta Binafsi ilichangia kiasi cha **Shilingi trilioni 32.6** sawa na **asilimia 85** ya matarajio ya **Shilingi trilioni 38.4**. Maeneo makuu yaliyowekezwa na sekta binafsi ni pamoja na maendeleo ya viwanda, shule binafsi, hospitali, hoteli, madini, usafirishaji na uhifadhi.

2.3. Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21) wenye dhima ya **“Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu”** umejielekeza katika kutekeleza vipaumbele vinavyohusu Miundombinu (Reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na nishati); Kilimo (Mazao, Mifugo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi); Viwanda; Madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii (Afya, Elimu na Maji) na miradi maalum ya kimkakati (Flagship Projects).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imechambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele; muda wa kati na mrefu wa utekelezaji wa kila kipaumbele; na uwajibikaji wa wataalamu wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huu umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo mpaka sasa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kissekta kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele yanayohusu miundombinu, kilimo, Viwanda na Huduma za jamii na ingependa kueleza yafuatayo;

2.3.1. Sekta ya Miundombinu

2.3.1.1. Barabara

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa, Serikali imepiga hatua kubwa na ya kuridhisha katika kuboresha miundombinu ya barabara nchini ukizingatia kuwa Nchi yetu yenye urefu wa mtandao wa barabara (vijijini, wilaya, mikoa na barabara kuu) unaokadiriwa

kufikia kilometa 143,279 ilikuwa na barabara za lami kilometa 9,781 tu mwaka 2015. Hii inaonyesha kuwa katika maisha yote ya nchi yetu hadi kufikia mwaka 2015 tuliweza kujenga barabara za lami kilometa 9,781 tu sawa na asilimia 7 ya mtandao wote wa barabara tulionao.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa inaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka mitano cha Mwaka 2015 hadi Machi, 2020 Serikali imeweza kujenga kilomita 3,537.0 za lami katika maeneo mbalimbali nchini, kilometa 82.6 za kupunguza foleni katika miji mikubwa na hadi kufikia mwezi Juni, 2020 barabara zenye urefu wa kilometa 1,298.44 zilikuwa zipo katika hatua ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Pamoja na ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami, Serikali imeweza kukarabati kilometa 300.9 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja makubwa 12. Kiasi cha **shilingi trilioni 8.60** kilitumika katika ujenzi huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya ya kuridhisha, bado kuna changamoto kubwa ya uwepo wa barabara bora na za kutosha nchini. Aidha, maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi hasa kipindi cha masika kutokana na ubovu wa barabara na madaraja au kutokuwa na barabara kabisa. Hali hii inapelekea kuongeza gharama ya maisha hasa kwa upande wa upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwa barabara ambazo zinazofungua fursa za kiuchumi na barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa lengo la kukuza shughuli za kilimo, biashara na uwekezaji mathalani barabara ya Songea – Muhukulu - Mkenda na upanuzi wa barabara inayoelekea katika mpaka wa Tanzania na Zambia (Barabara Igawa-Tunduma; Matai – Kasesha border;) na nyinginezo. Hivyo ni

mategemeo ya Kamati kuwa Mpango wa Tatu Maendeleo utazingatia maoni haya ya Kamati.

2.3.1.2. Reli

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kujenga Reli mpya ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR) itakayo gharimu **Dola za Kimarekani Bilioni 7.69** kutoka Dar es salaam hadi Mwanza. Reli hii itakapokamilika itasaidia sana kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Mikoani na nchi za jirani zinazotumia bandari zetu na hivyo kuchochea kilimo, uzalishaji, biashara na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na Serikali kwenye miundombinu ya reli nchini kwa kukarabati reli (DSM-Mwanza; DSM-Tanga-Arusha), ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa mapya. Hata hivyo pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana, Kamati inaishauri Katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo Serikali izingatie mambo yafuatayo;

- i. Serikali ikamilishe haraka mapitio ya Mkataba na Sheria inayosimamia Reli ya TAZARA ili kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha Tanzania kuisimamia na kuiendesha reli hiyo pamoja na miundombinu yake kwa upande wa Tanzania;
- ii. Serikali ione uwezekano wa kuunganisha reli zake zote ili kuwa na mtandao mmoja wa reli ikiwemo ujenzi wa reli ya TAZARA kutoka Tunduma kwenda Kasanga;
- iii. Serikali itafute haraka fedha za kukamilisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha SGR kutoka Makutupora-Tabora-Isaka, Isaka – Kigoma, Isaka – Katavi-Kalema ambazo hazijaanza kujengwa. Mapato yatakayopatikana kutoka katika uendeshaji wake yatumike kulipia deni la mkopo wa ujenzi;
- iv. Serikali ione uwezekano wa kujenga Bandari kavu katika Mkoa ya Mbeya, Kigoma, Mwanza, Arusha na Shinyanga (Isaka) ili mizigo ya

- nchi jirani (On Transit Cargo) itakayosafirisha na reli zetu ipokelewe na kupakiwa huko badala ya kuwalazimu kuja Dar es salaam; na
- v. Serikali ione uwezekano wa kuunganisha Eneo Maalum la uwekezaji la Bagamoyo na Reli ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa zitakazozalishwa hapo.

2.3.1.3. Usafiri wa Anga

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha usafiri wa anga nchini kwa kukarabati viwanja vya ndege, kujenga viwanja vipya katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kununua na kufunga Rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraia katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, Songwe na Mwanza. Hatua hii imeweza kuboresha usafiri wa anga kuongeza hamasa ya maendeleo hasa katika sekta ya usafirishaji, biashara na utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha Shirika letu la ndege (ATCL) kwa kununua ndege 8, kuendelea na mchakato wa kununua ndege nyingine 3 na imepanga kununua ndege nyingine zikiwemo ndege za mizigo. Kamati inaishauri ATCL kuongeza safari zake za ndani pamoja na kusafirisha mizigo zaidi hasa mbogamboga, maua nyama na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje. Aidha, serikali iongeze kasi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Songea, Iringa, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga.

2.3.2. Sekta ya Nishati

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio makubwa katika usambazaji wa umeme vijijini kutoka vijiji 2,018 mwaka 2015 hadi kufikia vijiji 10,018 Desemba, 2020. Aidha ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme katika maeneo mbalimbali nchini umefanyika. Pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto ya uunganishwaji wa umeme katika nyumba (Households connection) ambao ni **asilimia 39.9** tu za nyumba katika maeneo ya mijini na **asilimia 24.3** tu ya nyumba maeneo ya vijijini. Pia, bado kuna upotevu wa umeme wakati wa usafirishaji kutoka eneo la

uzalishaji hadi eneo la usambazaji. Kamati inaishauri Serikali kutafuta njia ya haraka ya kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga ifikapo mwaka 2020/21 uzalishaji wa umeme nchini uwe umefikia kiwango cha 4,915 MW kutoka 1,308 MW mwaka 2015/16. Hata hivyo hadi kufikia mwaka 2019/20 uzalishaji umefikia kiwango cha 1,602.3 MW tu. Ni matumaini ya Kamati kuwa ukamilishaji wa Mradi wa kipekee wa kuzalisha umeme wa Maji wa Julius Nyerere utakaozalisha 2,115 MW, Mradi wa Rusumo 80 MW; Kinyerezi I Extension 185 MW; Mradi wa Ruhudji 358 MW na Mradi wa Rumakali 222 MW itaweza kusaidia kupunguza kiwango cha upungufu wa umeme na hivyo kufikia lengo lililokusudiwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa uhakika wa umeme wa gharama nafuu kwa wenye viwanda na wananchi.

2.3.3. Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo ndio msingi wa uchumi wa Viwanda kwasababu ndio sekta zalishi ya malighafi ambazo zinatumiwa viwandani na ndiyo yenye kuajiri zaidi ya **asilimia 66** ya wananchi wa Tanzania. Kilimo si tu kina athari kubwa katika Uchumi wa Nchi lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa ilikuwa ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka **asilimia 3.4** kwa mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 7.6** kwa mwaka 2020. Hata hivyo, hadi sasa ukuaji wa Sekta ya kilimo umefikia **asilimia 4.4** kwa mwaka 2019 chini ya lengo lililokusudiwa la **asilimia 7** kwenye Mpango wa Pili. Aidha uchangiaji wa Pato la Taifa umeweza kufikia **asilimia 26.6** na hivyo kushindwa kufikia lengo la uchangiaji wa **asilimia 29.4** kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa bado utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo ipo nje ya malengo tuliyojiwekea hasa kwa upande wa

uzalishaji wa mazao ya thamani. Bado kuna changamoto ya kufikia malengo ya kuuza mazao yetu nje ya nchi. Aidha, Kwa upande wa kilimo cha Umwagiliaji kimeongezeka kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020, ukilinganisha na lengo la mpango wa Pili wa kufikia hekta 700,000.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutofikia kwa malengo kwenye sekta ya kilimo, Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, kujenga viwanda vya kuongeza thamani mazao. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali wakati ikitekeleza Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo izingatie yafuatayo;

- i) Kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi;
- ii) Kuendelea kuhamasisha na kukuza kilimo cha umwagiliaji;
- iii) Kuboresha masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;
- iv) Kuendelea kufanya utafiti kwa lengo la kuzalisha mbegu bora za asili zinazopatikana kwa bei nafuu kwa wakulima;
- v) Kuendelea kuhamasisha upatikanaji wa pembejeo na madawa ya kilimo kwa wakati na gharama nafuu;
- vi) Kuanzisha vituo/masoko ya kukusanyia au kufanyia mauzo ya mazao katika kila wilaya na baadae Kata ili kuwapunguzia wakulima gharama kutafuta masoko. Aidha, Vituo hivi viunganishwe na Soko la Mazao (Tanzania Mercantile Exchange – TMX);
- vii) Kuendelea na utekelezaji wa program mbalimbali za kuboresha shughuli za Kilimo hasa ile ya ASDP II;
- viii) Serikali ikamilishe haraka mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na viwanda vya samaki; na

- ix) Kuboresha utaratibu wa Stakabadhi ya mazao gharani na uhusishe mazao yote ya biashara ili kurahisisha mazao hayo kuuzwa katika soko la mazao (TMX)
- x) Serikali ifanyie ukarabati wa haraka machinjio za kisasa (arbortour) na kupata ithibati (hati ya ubora) kwa nyama inayozalishwa nchini ili kuwezesha kuweza kuuza nyama yetu moja kwa moja katika masoko ya Ulaya, Asia na Uarabuni badala la kutegemea kupitia nchi jirani;
- xi) Serikali ianzishe hapa nchini Masoko ya Mazao Makuu ya Biashara kama vile Chai, Kahawa, Pareto na Kakao.

2.3.4. Sekta ya Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mazingira bora yaliyowezesha kuanzisha viwanda vingi nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiasi cha viwanda 8,477 vimeanzishwa. Kati ya viwanda hivyo, 201 ni vikubwa, 460 vya kati, 3,406 ni vidogo na 4,410 ni vidogo sana na kupelekea ajira katika viwanda kuongezeka kutoka 254,687 mwaka 2015 hadi 482,601 mwaka 2019. Ongezeko la idadi ya viwanda na uzalishaji imewezesha nchi yetu kuweza kujitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zikiwemo saruji, marumaru, nondo, vifaa vya umeme, mabomba ya plastiki, mahindi, mchele na vyandarua. Haya ni mafanikio yanayotia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, Ili kulinda viwanda vyetu na kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya Viwanda ni vema Serikali ikaja na mkakati utakaoviwezesha Viwanda vyetu vya ndani kuwa shindani na kuzalisha Zaidi. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi (Dumping) pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kuwezesha Biashara (Business Facilitation Act) pamoja na Sheria ya

Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act) kabla ya Julai 1, 2021.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Mipakani yanatoa mchango mkubwa sana wa uchumi kupitia biashara. Mfano halisi ni Mipaka ya Namanga na Tunduma. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya mipaka yetu na nchi jirani bado hajaweza kuleta mchango unaostahili wa manufaa ya kibiashara na kiuchumi. Kwa mfano Nchi yetu imepakana na nchi ya Msumbiji katika mkoa wa Ruvuma. Kwa kutambua umuhimu wa eneo hili, Serikali imejenga Soko la Kimataifa la Mkenda, ambalo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ubovu wa barabara ya Songea – Mhukulu – Mkenda (Border) soko hili halijaweza kufanya kazi. Mpaka wa Tanzania na Msumbiji Mkoani Ruvuma katika eneo la Mkenda unaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kusini mwa nchi yetu endapo utaboreshwa kwa kujengewe miundombinu ya muhimu hasa barabara.

Mheshimiwa Spika, Ili nchi yetu iweze kuwa na ushindani wa Kibiashara katika ukanda wa SADC, EAC, Africa na Dunia kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo inazingatia yafuatayo;

- i. Kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kuchakata mazao ya mifugo na mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kuyatafutia masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi yetu;
- ii. Serikali ikamilishe haraka uanzishwaji wa masoko ya mipakani ikiwemo kuanza matumizi ya Soko la Mkenda lililopo katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji Mkoa wa Ruvuma (Mpaka huu umesahaulika sana);
- iii. Serikali ianzishe Viwanda vya Dawa na Vifaa tiba kwa ajili ya matumizi yetu na kuuza katika nchi cha SADC, Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla; na
- iv. Serikali ikiwezeshe Kiwanda cha *Biotech Production Limited* kilichopo Kibaha ili kiendeleo kuzalisha viluilui wa kuuza vijidudu wa mbu

wanaoeneza malaria na magonjwa mengine ili kutokomeza kabisa malaria nchini na hivyo kupunguza vifo na gharama kubwa inayotumika kutibu ugonjwa huu.

2.3.5. Sekta ya Ardhi na Mazingira

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu katika kuleta maendeleo. Hivyo kuna umuhimu wa kuzingatia upatikanaji wa ardhi na haki ya kuitumia katika maendeleo. Aidha, takwimu za sasa zinaonyesha kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa **asilimia 3.1** kila mwaka na hivyo kupelekea mahitaji makubwa ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na uwekezaji. Aidha, takribani ya **asilimia 70** ya watu wa Tanzania wanaishi maeneo ya vijijini wanategemea ardhi katika upatikanaji wa mahitaji yao ya maisha. Hali hii imepelekea kuwa na migogoro mikubwa ya ardhi pamoja na uharibifu mkubwa wa misitu (*Deforestation*) na vyanzo vya maji (source of water).

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa Mpango tunaotekeleza sasa haujaweza kusaidia katika kutatua matatizo yanayohusu ardhi na usimamizi wa mazingira. Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuna kuwepo mipango ya matumizi bora ya ardhi, uhifadhi wa mazingira na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hata hivyo nguvu zaidi inahitajika ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu ambao hadi mwaka 2019 wamefikia takribani watu milioni 55.9. Serikali lazima ihakikishe utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa upande wa vijiji, wilaya na mikoa unakamilika haraka, pia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya utatuzi wa migogoro ya ardhi yanatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, kwa upande wa mazingira, Serikali ihakikishe inaendeleza juhudi za kuhamasisha utunzaji wa mazingira ikiwa pamoja na kusimamia programu na sera za usimamizi wa mazingira, mafunzo ya uchambuzi na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

2.3.6. Sekta Utalii

Mheshimiwa Spika, Tanzania ndio nchi pekee duniani ambayo imetenga eneo lake kubwa kiasi cha asilimia 25 kwa ajili shughuli za kuhifadhi na kuendeleza shughuli za utalii kama vile hifadhi ya Taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi. Aidha sekta hii imeendelea kufanya vizuri katika kuchangia Pato la Taifa (asilimia 17.7) pamoja na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nje (asilimia 24). Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inaona kuwa juhudi mahususi zinahitajika ili tuweze kufikisha malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa upande wa kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni 1.7 na Mchango katika Pato la Taifa kufikia asilimia 18.3. haya yote yanaweza kufikiwa kwa :-

- i. Kuendelea kuhamasisha na kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi;
- ii. kuongeza bidhaa za huduma na utalii pamoja na kuendelea kuaninisha maeneo mapya ya utalii;
- iii. kuboresha miundombinu katika hifadhi za taifa, maeneo tengefu na maeneo ya uhifadhi; na
- iv. Kuendelea kuboresha mafunzo yanayotolewa na vyuo vya utalii.

2.3.7. Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2019 Sekta ya madini imekuwa kwa wastani wa **asilimia 8.0** na kuchangia Pato la Taifa kwa **asilimia 5.2** mwaka 2019/20 kutoka **asilimia 4.6** kwa mwaka 2015/16 na hivyo kufikia malengo tuliojiwekea kwenye Mpango wa Pili wa Taifa. Aidha mapato ya fedha kigeni kutoka kwenye mauzo ya madini yameongezeka kutoka **Dola za Kimarekani milioni 1,912 (trilioni 4.46)** kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia **Dola za Kimarekani Milioni 2,898.8 (trilioni 6.76)** mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali imefanikiwa kulipa fidia katika eneo linalotakiwa kujengwa kiwanda cha ubia cha kubadilisha gesi asilia iwe katika hali ya kimiminika (LNG). Kamati inaishauri Serikali kukamilisha kwa haraka majadiliano na wabia walioonyesha nia ya kuwekeza katika mradi huu ambao ni wa muda mrefu. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya usambazaji wa gesi asilia viwandani ili kupunguza gharama za uzalishaji na kupunguza matumizi ya mkaa majumbani.

Mheshimiwa Spika, hatua hii nzuri imefikiwa baada ya kuwepo na ushiriki wa Serikali katika Tasnia ya uchimbaji wa madini uliochangiwa na mabadiliko makubwa ya sheria zinazosimamia uchimbaji wa madini kama vile Sheria ya Madini, 2017 (The Minerals Act, 2017), Sheria ya Mamlaka ya Kudumu ya Tanzania juu ya Rasilimali na Utajiri wa Nchi (Natural Resources (Permanent Sovereignty) Act of 2017, Tamko la Uanzishwaji wa Mashirika ya Umma (The Public Corporations(establishment Amendment) Order, 2015) na Sheria ya Mafuta (The Petroleum Act of 2015). Hatua hii pia, imetoa mamlaka kwa shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kushiriki katika biashara za madini na nishati hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri hasa pamoja na ile ya kuanzishwa kwa Kampuni Mpya Twiga Minerals Corporation inayomikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (Hisa **asilimia 16**) na Kampuni ya Barrick (Hisa **asilimia 84**) ambapo imetoa gawio la shilingi Bilioni 100. Pia, kuanzishwa kwa kampuni mpya ya Tembo Nickel Corporations Limited ambapo Tanzania ina hisa ya umiliki wa **asilimia 16**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii nzuri ni wakati wa mashirika ya STAMICO na TPDC kuhakikisha yanafanya biashara na kupata faida na kutoa gawio linalostahili kwa Serikali na hivyo kuchangia Mapato. Aidha, bado kunahitajika upatikanaji wa takwimu sahihi za mapato yatokanayo na shughuli za uzalishaji wa gesi pamoja na makinikia yake.

2.3.8. Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu

2.3.8.1. Afya

Mheshimiwa Spika, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kwa kujenga zahanati, vituo vya Afya na Hospitali nyingi katika maeneo yote nchini. Serikali pia imeweza kuongeza idadi ya Watoa huduma wa afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano imepungua kutoka 67 kila vizazi 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 50 katika kila vizazi 1,000 mwaka 2019/20 hata hivyo ikiwa chini ya lengo la kufikia vifo 45 tu, Idadi Vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua ilipungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 321/100,000 mwaka 2020 hii ikiwa ni chini ya lengo la kufikia vifo 250 tu iliyowekwa kufikiwa katika Mpango wa Pili ifikapo mwaka 2021. Serikali pia imeongeza upatikanaji wa mashine za kisasa za kupima ugonjwa wa kifua kikuu (TB) (GeneXpert) kutoka 65 mwaka 2015/16 hadi mashine 239 mwaka 2020 (Machi, 2020), vifo vya malaria vimepungua kutoka watu 6,311 mwaka 2015 hadi 2,079 mwaka 2020 (Machi, 2020).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya bado kuna changamoto za upatikanaji wa vifaa tiba vya kutosha kama vile X-Ray machines, MRI, Mashine ya kutibu saratani (Chemotherapy) katika baadhi ya Hospitali na Taasisi za Afya kama vile Ocean Road Cancer Institute, Hospitali za Rufaa na Hospitali za Mikoa. Aidha, bado kuna changamoto katika usambazaji na usimamizi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali zetu nchini pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya Afya katika baadhi ya maeneo nchini ambayo yalijengwa kwa nguvu za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua madhubuti na zinazoendana na mazingira ya nchi yetu katika

kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19. Hatua hizi madhubuti zimewezesha nchi yetu kutopata athari kubwa za kiuchumi kwa kuruhusu wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za kila siku. Msisitizo ukiwa ni kufuata maelekezo yote yanayotolewa na Serikali na Wataalamu wa Afya ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya kuridhisha yaliyopatikana katika Sekta ya Afya, Kamati ingependa kutoa maoni yafuatayo ili Serikali iyazingatie wakati wa kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo;

- i. Serikali ikamilishe haraka ujenzi wa Maboma ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali ambazo bado ni maboma na kuzipatia watumishi, dawa na vifaa tiba;
- ii. Serikali itenge fedha za kutosha kwa bohari kuu ya madawa (MSD) ili iweze kusambaza dawa na vifaa tiba nchini pamoja na kuiwezesha kusambaza dawa na vifaa tiba katika nchi za SADC na hivyo kujiongezea mapato;
- iii. Serikali ihakiki madeni ya MSD na ifanye utaratibu wa kuyalipa ili iweze kuendelea kusambaza dawa na vifaa tiba;
- iv. Pamoja na kupambana na ugonjwa wa Covid-19, Serikali iendeleo kutilia mkazo katika kupambana na magonjwa mengine hasa Malaria na Kansa magonjwa ambayo yanachangia sana katika idadi ya vifo nchini; na
- v. Serikali itekeleze agizo la Mheshimiwa Rais la kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kununua dawa inayozalishwa na kiwanda cha Biotech Production Limited kwa ajili ya kuua viluilui wanaoua vijidudu wanaoeneza malaria pamoja na magonjwa mengine kama Dengue, Zika, Matende, Homa ya Manjano (Yellow Fever), Chikungunya na Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley)

2.3.8.2. Elimu

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa, Serikali imepiga hatua kubwa katika kuboresha elimu nchini kwa kuongeza uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari baada ya kupitisha Sera ya Elimu bila Malipo. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa upande wa shule za msingi udahili (Gross Enrollment Ratio) umeongezeka kutoka **asilimia 91.3** kwa mwaka 2015 hadi kufikia **asilimia 110.3** kwa mwaka 2019. Kwa upande wa shule za sekondari (O-level) udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka **asilimia 36** mwaka 2016 hadi kufikia **asilimia 43.9** mwaka 2020. Aidha, sambamba na udahili, Serikali imeweza kuongeza ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara, nyumba za walimu, utengenezaji wa madawati na kupunguza uhaba wa vitabu katika Shule za Msingi na Sekondari. Pia Serikali imeweza kuongeza idadi kubwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015/16 hadi wanafunzi 132,392 mwaka 2020. Pamoja na mafanikio haya, changamoto iliyopo ni kuona kwa namna gani mikopo ya elimu ya juu itapatikana kwa wanafunzi wote wanaomaliza elimu ya sekondari ili waweze kuendelea elimu ya chuo kikuu. Aidha, bado kuna mahitaji ya walimu wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu ili kuweza kukidhi utolewaji bora wa elimu kwa wanafunzi wanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa hamasisha na kujenga vyuo vya ufundi stadi kwa lengo la kutoa elimu itayowawezesha wahitimu kujijiri wenyewe hasa katika maeneo yanayohusu mafundi mchundo, maafisa ugani, stadi za mikono na ujasiliamali.

2.3.8.3. Maji

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwekeza kwenye maendeleo ya rasilimali maji na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa gharama nafuu. Hata hivyo pamoja na juhudi hizi bado hatujaweza kufikia malengo ya Mpango wa Pili ya kutoa huduma ya maji safi na salama kwa **asilimia 80** kwenye maeneo ya vijijini na **asilimia 90** kwenye maeneo ya mijini. Takwimu zinaonyesha kuwa hali upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka **asilimia 47** mwaka 2015 hadi **asilimia 70.1** mwaka 2020 na mijini imeongezeka kutoka **asilimia 74** mwaka 2015 hadi **asilimia 84** mwaka 2020. Hivyo Serikali inahitajika kufanya juhudi zaidi za kuhakikisha kuwa malengo ya Mpango wa Tatu kwenye miradi ya maji yanafikiwa ikiwa pamoja na kuongeza usimamizi wa miradi ya maji hususan kwenye Halmashauri zetu nchini. Aidha, wizara ya Maji iendelee kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwa kiwango kinachotakiwa na kwa utaalum madhubuti ikiwa ni pamoja na:-

- i. Kulinda vyanzo vya maji vilivyopo kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji;
- ii. Kuweka mizania sahihi ya mgao wa fedha za mfuko wa maji vijijini na mijini; na
- iii. Kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maji vijijini ili kuhakikisha kwamba inakuwa na tija iliyokusudiwa.

2.3.8.4. Mapitio ya Sera ya Kuondoa Umaskini

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya hatua kubwa ya kupiga maendeleo ni kuona kwa namna gani ukuaji wa uchumi unasaidia kuondoa umaskini wa kipato. Takwimu zinaonyesha kuwa viashiria vya umaskini yaani; umaskini wa kipato (umaskini wa mahitaji ya msingi), pengo la umaskini; na tofauti ya kipato utagundua kuwa bado jamii ya wanaoishi vijijini ndio imeendelea kuathirika na

viashiria vya umaskini. Mfano, takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa msingi (**income poverty**) kwa Dar es Salaam ni **asilimia 8**, maeneo mengine ya mijini ni **asilimia 15.8** na maeneo ya vijijini ni **asilimia 31.3**; aidha, pengo la umaskini (**poverty gap**) kwa Dar es Salaam ni **asilimia 2**, maeneo mengine ya mjini ni **asilimia 3.5** na vijijini ni **asilimia 7.4**; na kwa upande wa tofauti ya kipato (**poverty inequalities**) imeendelea kuwa kubwa kati ya jamii inayoishi mjini na ile ya vijijini. Kwa takwimu hizi utaona bado ukuaji wa uchumi wetu unahitajika kutatua tatizo la umaskini hasa kwa jamii ya vijijini. Ni mategemeo ya Kamati kuwa ukuaji wa uchumi uliosababisha Tanzania kuwa Nchi ya kipato cha kati (middle-income-country) utasaidia kuimarisha Pato la Mtu hasa kwa jamii ya vijijini. Hatua hii inaweza kufikiwa ikiwa Serikali itahakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unabebwa zaidi na sekta zinazohusisha idadi kubwa ya watu mathalani sekta ya kilimo na viwanda ili ukuaji huu uweze kutiririka na kuwafikia wananchi walio wengi vijijini. Kwa hali ilivyo sasa ukuaji wetu wa uchumi unategemea sekta za ujenzi, mawasiliano, na huduma za fedha n.k ambazo zinajumuisha idadi mdogo ya watu na pia shughuli nyingi za sekta hizi zinafanyika katika maeneo ya mjini tu ambapo kuna idadi ndogo ya watu

3.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22- 2025/26)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua kwa kina mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa Tatu Maendeleo wa Taifa (2021/22-2025/26) wenye dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.*** Uchambuzi wa Kamati umejielekeza kwenye maeneo ambayo hayakufanya vizuri kwenye Mpango wa Pili na nini kifanyike kwenye Mpango huu wa Tatu; uzingatiaji wa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 tuliojiwekea; Mpango Mkakati wa Maendeleo wa muda Mrefu (Long Term Perspective Plan), Hotuba ya Rais alipokuwa akizindua Bunge la 12 pamoja

na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025. Hivyo ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itazingatia maoni na ushauri huu wakati wa maboresho ya Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

3.1. Malengo na Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia na kuchambua Mpango huu ambao umeainisha maeneo makuu yafuatayo;

- i) kuchochea uchumi shindani na shirikishi;
- ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma;
- iii) kukuza biashara
- iv) kuchochea maendeleo ya watu; na
- v) Kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuainisha maeneo haya, jambo la msingi ni kuona Mpango huu unatimiza shabaha zake zilizoainishwa ifikapo mwaka 2026 hasa katika upande wa ukuaji wa uchumi kufikia asilimia 8, sekta binafsi kuzalisha ajira milioni nane na akiba ya fedha ya kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Aidha, mpango huu pia ujielekeze kujibu changamoto zilizosababisha kutofikiwa kwa baadhi ya malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo.

3.2. Uchambuzi na Vyanzo vya Mapato vya ugharamiaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya mpango wa Tatu wa Maendeleo kwa kiasi kikubwa utategemea upatikanaji wa rasilimali fedha na usimamizi wa matumizi ya fedha. Ugharamiaji wa mpango umegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu; **kwanza**, mapato kutoka Serikali kuu yatakayotokana na mapato ya kodi, yasio ya kodi; **Pili**, Mikopo (ndani na nje); **Tatu**; Sekta Binafsi kutoka ndani na ile inayotokana na uwekezaji kutoka nje (Foreign Direct Investment). Mpango huu utagharimu kiasi cha shilingi **trilioni 114.8** ukilinganisha na shilingi **trilioni 107** zilizotarajiwa kugharamia Mpango wa Pili (**Ongezeko la trilioni 7.8**). Kati ya fedha hizo, Serikali itatoa kiasi cha

shilingi **trilioni 74.2 (Ongezeko la trilioni 15.2)** ikiwa sawa na kuchangia **trilioni 14.84** kila mwaka; na sekta binafsi itatoa kiasi cha shilingi **trilioni 40.6 (pungufu ya shilingi trilioni 4)** katika kugharamia utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu inayotufanya tusifikie malengo ya mpango ni kutopatikana kwa rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mpango. Tathmini inaonyesha kuwa bado fedha zilizotengwa kwenye utekelezaji wa Mpango wa Pili zilikuwa chini ya lengo na wakati mwingine fedha zilizotengwa hazikuelekezwa kwenye maeneo ya kipaumbele cha Mpango. Hivyo, Kamati inaona kuwa Serikali iongeze juhudi za upatikanaji wa fedha za ziada za ugharamiaji wa miradi ya maendeleo ukizingatia kwa upande wa sekta binafsi kiwango kimeshuka kwa kiasi cha **trilioni 4** na kwa Serikali kimeongezeka kwa **trilioni 15.2**. Hivyo, ni vema Mpango huu wa Tatu ukajielekeza kutatua changamoto za upatikanaji wa fedha za kugharamia Mpango ili kufikia malengo na shabaha tuliyojiwekea.

Jedwali Na. 1: Ugharamiaji wa Mpango wa Pili ukilinganisha na Mpango wa Tatu (Trilioni)

Na.	Bajeti	Serikali	Sekta Binafsi	Jumla ya Bajeti yote
1.	Jumla ya Fedha zilizotengwa kugharamia Mpango wa Pili 2016/17 -2020/21	59	48	107
2	Jumla ya Fedha zilizotengwa kugharamia Mpango wa Tatu 2021/22 -2025/26	74.2	40.6	114.85
3	Asilimia Ongezeko/Punguzo	25.8	(8.8)	6.7

3.3. Upatikanaji wa Mapato na Mwenendo wake

Mheshimiwa Spika, Mpango huu utagharamiwa na mapato yatakayotokana na mapato ya kodi, yasio ya kodi pamoja na Mikopo (ndani na nje). Hivyo, Serikali ijielekeze katika kuhakikisha kodi, ada na tozo zinalipwa pamoja na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuweza kupata kiasi cha **trilioni 14.84** kila mwaka. Aidha, mwenendo wa upatikanaji wa Mikopo yenye masharti nafuu na misaada unaonyesha kushuka kutoka mikopo ya **shilingi trilioni 1.75** mwaka 2021/22 hadi kufikia **shilingi trilioni 1.596** mwaka 2025/26; Na misada kutoka **shilingi trilioni 1.12** mwaka 2021/22 hadi kufikia **shilingi milioni 520,261**. Hali hii inaashiria kuwa **“Watanzania lazima tulipe kodi kwa maendeleo ya Taifa letu”**

Jedwali Na. 2. Baadhi ya vyanzo vya mapato na mwenendo wake

Mwaka	2021/22	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Mapato ya Kodi	22,097,676	24,104,998	26,269,832	28,574,140	30,658,286
Mapato yasio ya Kodi	3,071,042	3,192,899	3,606,752	3,885,388	4,299,588
Mapato ya Halmashauri	863,858	917,022	975,558	1,043,847	1,101,700
Misaada	1,127,188	959,108	865,416	745,557	520,261
Mikopo ya Masharti nafuu	1,757,802	1,706,574	1,663,106	1,627,871	1,596,144
Mikopo ya Biashara	2,352,107	2,421,900	1,840,650	1,745,450	1,646,775

Chanzo: Wizara ya fedha namipango

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti ya kuziba mianya ya ukwepaji kodi ili kukahikikisha uhakika wa ukusanyaji wa mapato ikiwa pamoja na kuongeza wigo wa mapato. Vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali inaweza kutumia ni mifuko maalum ya serikali, mikopo maalum ya maendeleo, hati fungani za miundombinu na mapato yatokanayo na sekta ya madini mafuta na gesi.

3.4. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati (Flagship Project).

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Tatu umejielekeza kukamilisha miradi ya kimkakati na kipaumbele ili kuhakikisha tunafikia malengo na shabaha ifikapo mwaka 2026. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza kwa kiwango kikubwa miradi ya Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji-Julius Nyerere MW 2,115; Uboreshaji wa Shirika la Ndege na kuendelea miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja; Ununuzi wa Meli; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere; Mnazi Bay kaskazini na ziwa Tanganyika; na kuendelea na mchakato wa kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua kubwa iliyofikiwa katika kupeleka umeme vijijini kupitia mpango wa usambazaji umeme vijijini (REA). Hata hivyo, Mpango huu wa Tatu ujielekeze zaidi kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme kwenye vitongoji na mitaa na maeneo yanayokua kwa kasi ili kuwafikia wananchi wengi pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo vya uchakataji wa mazao vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu ujielekeze katika kuondoa urasimu wa utekelezaji wa miradi ya maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ/SEZ) hasa kwa upande wa kukamilika mikataba na ulipaji wa fidia mfano mradi wa bagamoyo, eneo la uwekezaji kigoma, Mtwara na mengine. Pia bado kuna uendelezaji hafifu wa maeneo ya Kanda maalumu za uwekezaji katika maeneo ya Dodoma, Ruvuma, Manyara, Mara, Manyoni na Tanga.

3.5. Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufadhili miradi ya maendeleo.

Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi kuwekeza.

Ushiriki wa Sekta binafsi katika miradi ya maendeleo unapunguza gharama ya Serikali katika kugharamia miradi ya maendeleo na pia inachochea kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Hata hivyo sekta binafsi bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali hasa zinazohusu maeneo yafuatayo :-

- i) Uwingi wa mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi;
- ii) Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi;
- iii) Uwingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja;
- iv) Kuboresha mazingira ufanyaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hizi ni baadhi tu ya changamoto zinazoikabili sekta binafsi katika ushiriki wa miradi ya maendeleo. Hivyo kuna umuhimu kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo kujielekeza kutatua changamoto hizi ikiwa pamoja na kuhuisha mwongozo wa ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini (Blue Print) kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa inayohusu biashara na uwekezaji. Aidha Muswada wa Sheria ya uwezeshaji wa Biashara (Business facilitation Act) uwasilishwe Bungeni haraka ili uweze kusaidia kutatua changamoto hizi.

3.6. Sekta za Huduma ya Elimu na Afya

Mheshimiwa Spika, Kama nilivyokwisha sema awali kwamba mpango huu una dhima ya ***Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu***. Hivyo ni wazi huwezi kuongelea maendeleo ya watu bila kutaja sekta za elimu, maji na Afya japo sekta zote za miundombinu na biashara nazo zina lenga maisha ya watu ila sekta hizi ni msingi kwa maendeleo ya watu.

3.6.1. Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa mpango wa pili limeonekana ombwe katika sekta yetu ya Elimu ambayo imeonekana kuzalisha wataalamu wasio endana na mahitaji ya

soko. Hii imesababishwa na mambo makuu matatu; **Kwanza**, ni mabadiliko ya uchumi wa Taifa na Dunia ambao unaenda kwenye mageuzi ya nne ya Viwanda (*Fourth Industrial Revolution “Digital Economy”*); **Pili**, ni uwekezaji mdogo kwenye elimu za Ufundi; na **Tatu**, ni mitaala yetu kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapungufu hayo Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya haraka ya mitaala yetu kabla ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango haujaisha na kufanya uwekezaji mkubwa katika vyuo vya ufundi na veta ili maendeleo ya viwanda yaendane na ujuzi. Aidha, kamati inaishauri serikali kufanya uwekezaji wa haraka katika miundombinu ya shule kwa sababu hivi sasa shue nyingi zimezidiwa kutokana na Sera njema kabisa ya Serikali ya awamu ya Tano ikiongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Elimu bila Ada “Free fee Education”.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna umuhimu wa kutathmini Mfumo na Mitaala ya Elimu yetu (Education Structure and Curriculum) ili kuona kama inaleta tija tunayoitegemea katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Ni lazima tufanye tathmini ili kuona je tunahitaji kuendelea kuongeza Idadi ya Vyuo Vikuu nchini na kuongeza Idadi kubwa ya wahitimu wa vyuo vikuu katika fani nyingi zaidi au tunahitaji kubadili mtazamo na uelekeo kwa kuwekeza zaidi katika Elimu ya kati ya ufundi stadi ili kuweza kupata wataalamu watakaoweza kujijiri wenyewe na wengine watakaotumika katika viwanda vyetu ambavyo vingi vipo katika kundi la viwanda vidogo na viwanda vidogo sana. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini hii haraka, ili tunapoanza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa 2021/22 – 2025/26 tuanze tukijielekeza katika mtazano mpya wenye lengo la kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kukuza biashara na kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya Elimu ya Juu kwamba Riba ya mikopo hii ipo juu sana na kiwango wanachokatwa kila mwezi ni kikubwa sana. Kamati inaishauri Serikali irejee upya viwango hivyo.

3.6.2. Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha kwa kasi Hospital za kanda za Rufaa, Mikoa, Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya. Katika Mpango huu wa Tatu, kama viashiria na malengo yaliyowekwa yatafikiwa basi nchi yetu itakuwa imepiga hatua kubwa katika kuimarisha utolewaji wa huduma ya Afya. Aidha, kasi hii iendane pia na ununuzi wa madawa na vifaa tiba, kuongeza watumishi wa afya kulingana na mahitaji, kuweka mkakati maalumu wa kupambana na magonjwa mbalimbali hasa yale yasiyo ambukiza ambayo matibabu yake yameendelea kuwa ya gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Mpango huu wa Tatu ujielekeze katika kuhakikisha kuwa majengo yote ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali yaliyoanza kujengwa (Maboma) yakamilishwe na kupatiwa vifaa tiba na watumishi kabla ya kuanza ujenzi mpya.

3.7. Tathmini, Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Mpango wa Tatu imeonyesha kwamba Serikali inakusudia kutumia Nyanja zote za utawala katika kusimamia utekelezaji. Hata hivyo kamati imebaini kwamba utaratibu uliopendekezwa haukufanya vizuri katika Mpango wa Pili kwa sababu hakukuwa na rasilimali za kutosha za usimamizi na ufuatiliaji na vilevile utembeleaji wa miradi haukufanyika kikamilifu. Tatizo hili linaweza kuwa kubwa kwa upande wa miradi inayotekelezwa na utaratibu wa *Force Account* ambapo hakuna fedha yoyote inatengwa ya tathmini na ufatiliaji

hivyo inaweza kusababisha tukawa na miradi mingi ambayo imetekelezwa kwa kiwango cha chini

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa mpango ni jambo muhimu sana ili kujua wapi tumetoka, wapi tulipo na wapi tuendako na hivyo kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa. Katika Mpango huu wa Tatu, Kamati inaishauri Serikali ijikite zaidi katika mambo yafuatayo:-

- i) Serikali ihakikishe kunakuwepo na upatikanaji wa taarifa endelevu za utekelezaji (miradi na bajeti) dhidi ya hatua au malengo ya mpango;
- ii) Serikali iweke utaratibu maalumu wa kuchanganua kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi zitakazokuwa zinawasilishwa kwa kila kipindi maalumu cha utekelezaji. Hatua hii, itasaidia kujua hatua inayofikiwa kwa kila mradi husika;
- iii) Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitoe takwimu sahihi za utekelezaji wa miradi ili kusaidia ufanyaji wa tathimini kwa ufanisi;
- iv) Serikali ihakikishe inatekeleza Mpango huu kulingana na Sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA (2021/22-2025/26)

4.1. Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi

Mheshimiwa Spika, kimsingi Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano umejielekeza katika kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazoweza kushindana kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa hizo ndani na nje ya

nchi. Lengo likiwa na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa shindani nje ya nchi. Kamati inaona kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunaanza na viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini.

4.2. Sekta ya Ujenzi

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi mikubwa ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa na makampuni ya nje na sababu zilizotajwa ni makampuni ya ndani kukosa mtaji na kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi husika ambayo hufadhiliwa kwa fedha za nje. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango mizuri ya kusaidia makampuni ya ndani kuweza kuwa shindani, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, utoaji wa vivutio vya kikodi kwenye mitambo inayotumika na vifaa vya ujenzi. Matumizi ya wakandarasi wa ndani badala ya wakandarasi wa nje yatainufaisha nchi kiuchumi kwa kuwezesha fedha kubaki nchini na kuchochea uwekezaji na uzalishaji na kuongeza mzunguko wa fedha.

4.3. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Miundombinu suala la msingi la kuzingatia ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya msingi inajengwa katika maeneo ya kimkakati ili Taifa linufaike na fursa na nafasi yake kijiografia (*Strategic Geographical Location*) ya kuzungukwa na kuhudumia nchi 6 zisizo na bandari (*landlocked countries*). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati mahsusi kutekeleza yafuatayo kwa kuzingatia malengo ya Mipango ya Maendeleo yaliyowekwa:-

- a) Kuanzisha na kukamilisha ujenzi wa barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za mijini na vijijini zenye jumla ya urefu wa km 8,506.

- b) Kugharamia uboreshaji wa miundombinu ya Reli ya TAZARA na Reli ya Kati kwa vipande vilivyobaki ili reli hizo ziwe na manufaa ya uchumi wa usafirishaji.
- c) Kupanua na kuboresha Bandari za Tanga na Mtwara, na Bandari za ndani za Mwanza, Kigoma na Itungi.
- d) Ununuzi wa haraka wa *Cranes* na *Converyer Belt* kwa ajili ya kupakia na kushusha shehena za mizigo kwenye Gati za Bandari ya Dar es salaam zilizokamilika. Ni vema zikanunuliwa haraka kwa sababu hivi sasa kazi kubwa inafanywa na Kampuni ya binafsi kwa gharama kubwa.

4.4. Ukarabati na ujenzi wa Viwanja vya Ndege

Mheshimiwa Spika, Kasi ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege nchini haiendani na kasi ya ununuzi wa ndege hali ambayo inaweza kusababisha kupungua wa miruko ya ndege (*few flight routes*) husika na hatimaye kuliletea hasara kubwa za kiuendeshaji Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Aidha, imedhihirika kwamba uwepo wa changamoto za kiusalama duniani kama vile milipuko ya magonjwa (Mfano COVID-19) husababisha safari za ndani za ndege ziwe na faida kuliko safari za nje. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege unaohusisha ujenzi, upanuzi na uboreshaji barabara za lami za ndege (*airport runways*) na uwekaji wa mifumo ya taa za kuongozea ndege (*aeronautical ground lighting systems*) ambazo zinaruhusu shughuli za viwanja wa ndege kuendelea kwa masaa 24.

4.5. Mzingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoiwezesha Sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, na viwanja vya ndege), kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuanzisha maeneo ya uwekezaji, kuweka sheria za fedha na kanuni zinazotabirika na kutekeleza mipango mbalimbali kama *ROAD map for improving Bussiness*

Environment Strengthening in Tanzania (BEST na Blue Print). Pamoja na juhudi hizo, Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji, Tanzania imeendelea kushuka kutoka nafasi ya 131 mwaka 2015 hadi 141 mwaka 2020 tofauti na lengo tulilojiwekea la kuwa wa 100 kati ya nchi 189 duniani katika jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kubainisha maeneo (indicators) ambayo nchi haifanyi vizuri na kuweka mikakati madhubiti ya kuboresha maeneo husika. Mikakati hiyo ihusishe pia namna bora ya kuunganisha mamlaka za udhibiti (Regulatory Authorities) chini ya **Regulatory Ombudsman** ambazo zinafanya majukumu yanayoshabihiana, pamoja na Wizara ya Fedha kukamilisha uanzishaji wa **Office of Tax Ombudsman** itakayoshughulikia malalamiko kuhusu kodi na ushuru suala ambalo ni muhimu katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

4.6. Ushirikishwaji wa Watanzania katika Miradi ya Maendeleo na Uwekezaji nchini (Local Content)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka sera na kutunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa watanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uwekezaji nchini kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi. Changamoto kubwa iliyopo ambayo hata Mipango ya Maendeleo ya Taifa haujaweza kutanzua kikamilifu ni kubainisha ushirikishwaji wa watanzania (local content) katika kila sekta badala ya kitaifa. Kamati inaona ni vema Serikali ikaliweka suala la Ushirikishwaji wa Wananchi wote kwenye shughuli za kiuchumi kwenye Sheria na Sera moja ya Ushirikishwaji au Uwezeshaji wa Wananchi ili iwe rahisi kusimamia, kufuatilia pamoja na sekta zote kuwajibika kwenye Sheria moja tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo hata ufuatiliaji unakuwa mgumu.

4.7. Uzingatiaji wa Mapinduzi ya Kidijiti (Digital revolution) katika Mipango ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Mapinduzi ya kidijiti (*Digitalization*) yamesababisha pamoja na mambo mengine wananchi kufanya miamala ya kibiashara na

kiuwekezaji kwa kutumia mitandao mbalimbali hususani mitandao ya simu, mitandao ya taasisi za fedha na kibenki na mitandao ya taasisi za serikali. Matumizi ya mitandao yamesababisha changamoto za ukwepaji wa kodi na utakatishaji wa fedha zilizopatikana kwa njia zisizo halali. Makampuni mengi ya kigeni na hata ya wazawa yamekuwa yakikwepa kodi kubwa kwa kutotoa takwimu sahihi za faida inayopatikana au kuhamisha faida kwa kampuni tanzu (*BEPS- Base Erosion and Profit Shifting*). Hivyo, Kamati inaishauri Serikali wakati tukiendelea kuboresha mifumo ya kieletroniki na matumizi ya mtandao katika kutekeleza shughuli za serikali na za sekta binafsi, ni vema tukaweka mikakati madhubuti (*National Digitilization Strategy*) ya kutumia fursa na kuzuia athari za matumizi ya mtandao hasa za kimapato na kiusalama pamoja na kuwapa mafunzo ya kidijiti wataalamu wetu

4.8. Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Bahari Kuu

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa kuandaa mkakati wa taifa wa uchumi wa bluu na kuipa uzito sula la uvuvi wa bahari kuu kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano awamu ya Tatu ili kuwa na uendelevu wa ukusanyaji wa mauzo nje ya nchi. Aidha, kutokana na ukubwa wa sekta hii na *complexity* ni vema Sekta Binafsi na watalaam wenye uzoefu wa eneo hili kushirikishwa kwa upana wake ili hatimaye kuleta mafanikio yanayotokana na sekta hii hasa ukizingatia soko kubwa la mazao ya baharini duniani.

4.9. Maboresho katika kituo cha uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilianzishwa ili kuratibu, kuhamasisha, kukuza na kuwezesha uwekezaji nchini Tanzania na kuishauri Serikali juu ya sera ya uwekezaji na mambo mengine yanayohusiana na uwekezaji nchini. Kimsingi, TIC ilianzishwa ili iwe *One-Stop Shop* kwa ajili ya kusaidia na kuharakisha uwekezaji nchini. Kamati imeelezwa kwamba kwa sasa kwa sehemu kubwa suala ya utoaji wa

maamuzi ya uwekezaji nchini limehamishiwa kwa Wizara, Idara, Wakala au Mamlaka husika na hivyo kusababisha kuongezeka kwa urasimu katika sekta ya uwekezaji. Mfano mzuri Kituo cha Uwekezaji ambacho kinafanya kazi kwa ufanisi kama One-Stop Shop ni *Rwanda Development Board*. Kamati inaona ni muhimu kwa serikali kuliangalia upya suala ya ufanyaji wa maamuzi kuhusu shughuli za uwekezaji na uongezaji tija kwa shughuli za TIC.

5.0. MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22.

5.1. Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/22 ulioandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia sera, vipaumbele, mpango mkakati wa Taasisi husika na maelekezo ya Serikali iliyopo wakati wa uandaaji, utekelezaji, uwasilishaji na utoaji taarifa wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kati ya masuala yaliyotiwa mkazo katika Mwongozo ni pamoja na uandaaji wa mipango na bajeti inayozingatia mahitaji halisi ya rasilimali fedha ikiwa ni kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima. Aidha, Maafisa masuuli na mipango wanatakiwa kutumia mifumo ya kielektroniki iliyopo ikiwa ni pamoja na mfumo wa uhasibu Serikalini (MUSE), mfumo wa ukusanyaji wa mapato na malipo ya mtandao (GePG), mfumo wa uingizaji wa takwimu za Bajeti ya Serikali CBMS na PlanRep.

5.2. Utekelezaji wa Bajeti katika Kipindi cha Nusu ya Kwanza ya Mwaka 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya shilingi **trilioni 34.87**. Kiasi hicho kinajumuisha, shilingi **trilioni 22.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **trilioni 12.77** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi **bilioni 32.14** ni fedha za ndani na shilingi **trilioni 2.73** ni fedha za nje. Aidha, Serikali ilipanga kukusanya mapato yake ya ndani kiasi cha Shilingi **trilioni 24.065** na kukopa katika vyanzo vya ndani na nje kiasi cha shilingi **trilioni 10.81** ambapo kati ya mikopo hiyo kiasi cha shilingi **trilioni 2.73** ni kutoka nje na shilingi **trilioni 8.08** ni kutoka katika vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 15.84** Hata hivyo kiasi cha fedha kilichokusanywa katika kipindi hicho kutoka vyanzo vya ndani na nje ni shilingi **trilioni 13.85** sawa na **asilimia 87.4** ya makadirio. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia shilingi **trilioni 10.46** sawa na **asilimia 89.0** ya lengo la kukusanya shilingi **trilioni 11.75** Kati ya mapato hayo: mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi **trilioni 9.06** sawa na **asilimia 89.7** ya lengo la kukusanya shilingi **trilioni 10.10**; mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa **shilingi trilioni 1.02** sawa na asilimia 83.6 ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 1.22**; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia **shilingi bilioni 376.5** ikiwa ni **asilimia 89.0** ya lengo la kukusanya shilingi **bilioni 422.8**.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo takwimu zinavyoonyesha hapo juu Serikali haikuweza kukusanya kwa asilimia mia moja (100%) mapato iliyopanga kukusanya katika kipindi hicho cha nusu mwaka. Kutofikia lengo la makusanya kuliathiri utekelezaji wa baadhi ya shughuli ambazo

ziligwa kutekelezwa katika kipindi husika. Ni maoni ya Kamati kuwa ili Serikali iweze kupunguza ama kuondoa kabisa changamoto hii ya kutofikia malengo ya makusanyo yake ni vema ikafanya yafuatayo;

- i. Kuhamasisha na kuhakikisha matumizi ya Risiti za Kielektroniki;
- ii. Kuboresha utaratibu wa kukusanya Kodi ya Majengo (Property Tax);
- iii. Kuboresha utaratibu wa kukusanya kodi ya ardhi;
- iv. Kuongeza kasi na kuboresha utaratibu wa kurasimisha biashara zisizo rasmi ili ziweze kuingia katika utaratibu wa kulipa kodi stahiki.
- v. Kuandaa Kanzidata ya Biashara zote za Mtandao (database of online businesses) na kusajili na kuzipa TIN biashara zote zinazofanyika katika mtandao;

5.3. Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2021/22 ndio bajeti ya kwanza inayoenda kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Tatu wa Taifa (2021/22-2025/26) uliobeba dhima ya **“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”**. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22 utajumuisha ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa 2021/22 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 36.2** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21 ya **shilingi trilioni 34.8**. Mapato ya ndani yanatarajia kuwa **shilingi trilioni 26.03** ikiwa ni sawa na **asilimia 72** ya bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **shilingi trilioni 21.46**, mapato yasiyo ya kodi yakijumuisha mapato ya halmashauri, mapato ya utalii na mapato mengine yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 4.56**. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha **shilingi trilioni 10.21** zikiwa ni fedha kutoka Washirika wa Maendeleo, fedha

zitakazo kopwa kwenye soko la ndani na mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mwongozo Serikali katika mwaka 2021/22 haitapokea Misaada ya Kibajeti kupitia utaratibu *General Budget Support* (GBS) kutokana na kufika ukomo wa Mkataba wa Programu ya GBS katika sekta ya Fedha na Uchumi kutoka Jumuiya ya Ulaya iliyojumuisha nchi za Denmark na Sweden. Badala yake fedha hizo zitakuwa zinapelekwa moja kwa moja kwenye Miradi suala ambalo sio preference ya Serikali kwa kuwa yenyewe ndio inayojua mahitaji halisi ya kimaendeleo na utoa fedha hizo kulingana na mahitaji. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika na kushawishi kuendelea na utaratibu wa awali wa GBS. Aidha, Serikali iendeleo kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondokana kabisa na utegemezi wa kibajeti ambao hupelekea kuchelewa kukamilika kwa utekelezaji wa miradi au kukwama kabisa. Aidha, msisitizo uelekezwe kwenye kuimarisha mifumo ya tehama katika ukusanyaji mapato kwa Serikali Kuu na Halmshauri, usimamizi madhubuti wa Sheria za Kodi, kuimarisha taarifa za walipa kodi kutoka katika kanzidata mbalimbali na utoaji wa elimu kwa walipa kodi ili kuwa na mapato endelevu pamoja na kuimarisha makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, eneo la maoteo ya Mapato na Matumizi limekuwa changamoto kubwa kwa nchi. Aidha, katika mwaka 2020/21, Serikali ilianza kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kibajeti hususan katika kukokotoa, kuandaa maoteo ya mapato na matumizi ili kuiwezesha Serikali kuwa na bajeti endelevu ambapo pamoja na mambo mengine tathmini hii itaiwezesha Serikali kubuni vyanzo vipya vya mapato. Aidha, uchambuzi wa kina wa matumizi ya Serikali utafanyika ili kuongeza ufanisi endelevu katika utekelezaji wa bajeti. Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hizi zitazaa matunda na hatimaye kuikwamua nchi kutoka kwenye utegemezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua inazoendelea kuchukua katika kuimarisha mapato yake na kudhbiti upotevu wa mapato na wakwepaji kodi ambapo mwezi Desemba, 2020 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiwango cha juu ambacho hakijawahi kukusanywa cha **shilingi trilioni 2.089**. Hatua hii sio ya kubeza hasa ukizingatia changamoto ya kiulimwengu iliyopo katika kuuwainisha mapato na matumizi ya nchi. Hata hivyo, Serikali imeweza kuongeza mapato yake ya ndani kutoka **shilingi bilioni 850** (2016/17) kwa mwezi iliyokuwa inakusanywa hapo nyuma hadi kufikia wastani wa **shilingi trilioni 1.5** kwa mwezi kinachokusanywa sasa hivi.

6.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imeusoma na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22 yanayotoa mwanga wa jinsi Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021/22 utakavyokuwa katika kuimarisha azma ya **“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”**. Kwa upande wa mwelekeo wa mpango, Serikali imepanga kujikita katika vipaumbele vya kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara na kuchochea maendeleo ya watu. Aidha, mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti unatoa taswira ya uandaaji wa mipango na bajeti itakayotumika katika kugharamia maeneo ya vipaumbele vitakavyotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo huu yameainisha maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na maafisa masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa, kutekeleza, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha vyanzo mbalimbali vya kugharamia mpango wa maendeleo wa mwaka 2021/22 ambavyo jumla vitatoa takribani **shilingi trilioni 13.25**. Hii ni sawa na **asilimia 37** ya bajeti yote. Aidha, Kamati imebaini kuwa bado serikali inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hali inayosababisha kuwepo kwa mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonyesha kuwa katika mpango uliopita, pamoja ya kuwa Serikali ilionyesha wapi itapata fedha katika kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kitaifa ya kimakakati, bado fedha hizo hazikupatikana kwa wakati uliopangwa au kutofika kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika. Kamati inashauri kuwa Serikali ijipange vyema kuhakikisha inasimamia ipasavyo mapato ya ndani, misaada, mikopo pamoja na sekta binafsi ili kuhakikisha inapata kiasi hicho cha fedha za kugharamia mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi mikubwa ya kielelezo, kamati inakubaliana na Serikali kwa kuweka miradi mikubwa kumi na saba (17) ya kielelezo kama kipaumbele kikuu kimojawapo katika mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21. Hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia na kutekeleza kwa mafanikio miradi mikubwa ya kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya Viwanda, Kamati inaipongeza serikali kwa kupiga hatua katika sekta ya viwanda na hivyo kuongeza fursa za ajira, uzalishaji na mapato. Sekta ya viwanda ni kichocheo muhimu katika maendeleo ya uchumi na ndio iliyobeba dhima ya Mpango wa Tatu wa maendeleo ya Taifa ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Aidha, Moja ya shabaha ya mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22 ni Uanzishaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa ndani kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini. Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba tunaanza na bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa kwa kutumia malighafi za ndani. Hivi sasa bidhaa hizo tunaziagiza toka nje kwa kutumia fedha zetu za kigeni. 3

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri serikali kundezeza mikakati mbalimbali ya kupanua sekta za viwanda vidogo vidogo, kuongeza thamani ya bidhaa zetu pamoja na kuongeza mauzo nje. Pia ni muhimu mpango huu ukajielekeza pia katika kufikilia namna mchakato wa ujenzi wa viwanda vipya, kufufua na kukarabati viwanda ambavyo havifanyi vizuri na kufufua vile vilivyokufa

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ujielekeze katika kufungamisha shughuli za kilimo pamoja na shughuli za viwandani. Uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi duniani zimepiga hatua za uchumi wa viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa ya kukuza uchumi wetu (Pato la Taifa) na ushindani wa kikanda na kimataifa kupitia sekta husika.

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora yatakayoivezesha Sekta binafsi kuwekeza pamoja na kufanya biashara kwa urahisi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya usafirishaji (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege); kuboresha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika; kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji; kuweka sheria za fedha na kodi zinazotabilika (zisizobadilika mara kwa mara); kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mali ghafi kwa ajili ya viwanda na sheria bora za ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na mikakati thabiti ya utekelezaji wa mradi kituo cha viwanda cha kurasini (Kurasini Logistic Hub) ambacho kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha ushirikano wa kibiashara kati ya Tanzania na Mataifa mengine, kupitia uwekezaji katika miundombinu ya biashara na ujenzi wa viwanda. Hivyo ni vema Serikali ikajikita katika kufuata mipango yake inayojiwekea kila mwaka ili kuwezesha utekelezaji na ukamilishwaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, Mpango huu wa maendeleo wa mwaka 2021/22 ujikite katika kutoa majibu ya changamoto ambazo

hazikutatuliwa katika mpango wa maendeleo wa Taifa uliopita wa mwaka 2020/21. Hii itaisaidia serikali kufanya tathimini na ufuatiliaji katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Aidha, Mpango huu ujikite katika kutatua changamoto zilizopo sasa za hali ngumu ya maisha na umaskini wa kipato.

7.0. MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni na ushauri huu uliojikita katika maeneo mahsusni, Kamati ingependa kutoa maoni ya jumla yafuatayo:-

- 7.1.** Serikali iendelee kutoa kipaumbele stahiki katika nishati mbadala kama vile joto ardhi, umeme wa upepo na umeme wa jua ili kuboresha uzalishaji na usambazaji wa nishati nchini.
- 7.2.** Serikali itatue haraka changamoto ya bei na kuchelewa kufika kwa pembejeo za kilimo katika maeneo mbalimbali, upatikanaji wa mbegu bora za mazao nchini na kuaandaa ramani itakayoonyesha ni mazao yanayoweza kustawi katika kila Wilaya nchini.
- 7.3.** Serikali iainishe Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao nje ya nchi kwa kuingia mikataba na wanunuzi au nchi ili ziweze kununua mazao yetu. Balozzi zetu ziongeze kasi katika utafutaji wa masoko ya mazao yanayolimwa hapa nchini na kuuzwa nchi za nje.
- 7.4.** Serikali iweke katika Mpango wake wa Miaka Mitano unaokuja mikakati ya moja kwa moja itakayowezesha zao la korosho na mazao yake (cashnut product and by product) pamoja na mazao mengine ya biashara kuongezewa thamani kwa kutengeneza bidhaa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwaongezea kipato wakulima, wafanyabiashara na Taifa kwa ujumla.
- 7.5.** Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ueleze kinagaubaga ni namna gani nchi yetu itavuna manufaa na kukabiliana na changamoto zinazoletwa na uchumi wa kidijiti (*Digital Economy*) huku tukiendelea kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;

- 7.6.** Serikali iendelee kuhamasisha malipo kwa njia ya kielektroniki (electronic payments) na kuandaa Kanzidata ya Biashara zote za Mtandao (database of online businesses) na kusajili na kuzipa TIN biashara zote zinazofanyika.
- 7.7.** Serikali iweke utaratibu mzuri utakaoboresha zaidi ufanyaji kazi wa biashara itokanayo na *Export Processing Zones* (EPZs) ili ilete faida iliyokusudiwa bila kuathiri viwanda na biashara za ndani.
- 7.8.** Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha Michezo ya kubahatisha (Gaming Sector) kuendelea kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi pasipo kuleta athari kubwa za kijamii na kitamaduni lakini kwa kuiwezesha iendelee kukua na kuwa endelevu.
- 7.9.** Serikali itatue changamoto zinazojitokeza kwenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.
- 7.10.** Serikali itoe Waraka utakaozitaka Ofisi na Taasisi za Umma kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kabla ya kutumia bidhaa za nje. Kwa mfano Taasisi zetu za Polisi, Jeshi la Wananchi, Idara ya Uhamiaji, Magereza kutumia bidhaa za ngozi (viati, mikanda, mabegi n.k) vinavyozalishwa katika kiwanda cha ngozi cha Karanga, kiwanda kinachomilikiwa na Magereza.
- 7.11.** Mifuko ya Jamii pamoja Taasisi kama vile JWTZ, Jeshi la Magereza zihamasishwe na kuwezesha ili ziwekeze katika kujenga Viwanda vya kuongeza thamani Mazao mbalimbali kama vile Parachichi, Michikichi, Korosho na mazao ya korosho (Cashewnut product and by product).
- 7.12.** Kamati inashauri Serikali kutafuta njia ya kupunguza kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya Bajeti kwa kupitia dhamana ya Serikali na hati fungani. Badala yake Serikali ijikite zaidi katika kuongeza udhamini wa wakopaji wadogo (credit gurantee schemes) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (lease finance). Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (Liberization of Capital Market) ili kupunguza athari za Serikali kukopa kwenye soko la ndani.

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha, Mawaziri, Manaibu Waziri, Mkatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe

20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

08 Februari, 2021